# Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Robo ya I, 2020/2021



*Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Dkt Serera katika ziara za kutatua kero za wananchi..*

UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI

**Robo ya I, 2020/2021**

**UTANGULIZI.**

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kama zilivyo Halmashauri nyingine nchini imejikita katika kutekeleza shughuli zake kwa kufuata Mpango Mkakati wake wa miaka mitano **2017/2018** hadi **2021/2022.**

Lengo la Halmashauri katika Mpango Mkakati wake ni kutoa huduma bora kwa wananchi wote bila upendeleo.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha **2020/2021**, Halmashauri imetekeleza majukumu mbalimbali ya kutoa huduma kwa wananchi kupitia Idara na Vitengo vyake.

Aidha katika kipindi hicho, Halmashauri imepokea fedha kutoka Serikali kuu kiasi cha shilingi **827,112,540.75** kwa ajili ya mpango wa elimu bila malipo **(233,398,455.75),** TASAF III (**480,514,085**) na Mradi wa wasichana rika balehe (TASAF AGYW) (**113,200,000**).

Kiasi cha shilingi **1,572,357,138** ni fedha za bakaa zilizoingia mwishoni mwa mwaka wa fedha **2019/2020** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekata za Afya, Elimu na TASAF.



Pichani kushoto ni moja ya madarasa yanayoendelea kujengwa katika shule ya msingi Sabasaba kwa fedha za EP4R kutoka Serikali kuu.

Pamoja na fedha hizo kutoka Serikali Kuu, Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imeweza kutoa fedha kiasi cha shilingi **34,000,000** kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na walemavu.



*Moja ya kikundi cha walemavu cha **Hapa Kazi** Mkoka kilichopatiwa mkopo.*

Ili kuunga mkono juhudi za wananchi katika kujiletea maendeleo yao Halmashauri imeweza kutoa bati **315** kwa ajili ya kuezekea madarasa **6**, ofisi **1** ya walimu na matundu **22** ya vyoo katika shule za msingi Chamwino (Mlali), Saigoni (Ngomai) na Manyata (Ngomai). Aidha Halmashauri imetoa fedha kiasi cha shilingi **22,000,000** kwa ajili ya kumalizia miundombinu ya mabweni katika shule za Sejeli na Kongwa sekondari .

Katika kukabiliana na changamoto ya madarasa katika shule ya msingi Sagara, Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali inaendelea na ujenzi wa madarasa **3** na ofisi **1** ya walimu.

Halmashauri inawashukuru wadau wote waliochangia na wanaoendelea kuchangia ujenzi wa miundombinu ya madarasa na ofisi katika shule hiyo na shule nyingine katika Wilaya.



*Madarasa yanayoendelea kujengwa kwa mapato ya ndani katika shule ya msingi Sagara*

Katika sekta ya afya, Halmashauri katika kipindi hicho imetoa fedha kiasi cha shilingi **2,575,000** kwa ajili ya kuweka madirisha ya alminium katika zahanati ya kijiji cha Chamae ambayo kwa sasa imeanza kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha Halmashauri inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya majengo katika hospitali ya Wilaya kwa kutumia fedha kutoka Serikali Kuu. Majengo yanaoendelea kujengwa ni pamoja na lile ya Mionzi, jengo la kufulia na jengo la kliniki ya Baba, Mama na mtoto. Majengo yote yapo katika hatua ya kupiga lipu.



*Jengo la kliniki na Baba, Mama na Mtoto (RCH)*


***Limeandaliwa na:***

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
S. L. P 57
**KONGWA**

Simu: +255 26 2370031
Nukushi: +255 26 2370031
E-mail: ded@kongwadc.go.tz
Tovuti: www.kongwadc.go.tz


**Ndani ya Jarida hili:**


| | |
|---|---|
| Mafanikio ya uboreshaji miundombinu ya Afya yadhihirika | 2 |
| Halmashauri yavuka malengo ya ukusanyaji mapato | 2 |
| Kero za wananchi zapatiwa majawabu | 2 |
| Wadau waungana kuweka mkazo kilimo cha korosho | 3 |
| Maandalizi ya uchaguzi mkuu yaendelea vyema Kongwa | 3 |
| Serikali yalipa milioni mia tano kwa kaya masikini | 3 |
| Wananchi waendelea kunufaika na mkopo wa 10% | 4 |


## Vipaumbele vya Wilaya

- *Kusimamia ubora wa elimu na kuongeza ufaulu*
- *Kutoa huduma bora kwa Wananchi bila upendeleo*
- *Kusimamia kwa karibu ubora wa miradi ya maendeleo ili thamani ya fedha ionekane*
- *Kubuni na kusimamia miradi ya kiuchumi ili kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Halmashauri kwa ujumla*

# Mafanikio ya uboreshaji wa miundombinu ya afya yadhihirika

Halmashauri kupitia Idara ya Afya inalo jukumu la kutoa huduma za afya kinga na tiba kwa wananchi kupitia vituo **69** vya kutolea huduma za afya (**60** vya umma, vituo **05** Mashirika ya Dini, **03** binafsi, **01** Shirika la Umma) na Maduka ya dawa muhimu **100** yanayo-milikiwa na watu binafsi.

Katika kipindi cha robo ya kwanza, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Idara ya afya ni haya yafuatayo:-

- Kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba kwa 94% na huduma za chanjo kwa 78% .

- Kutokuwepo kwa vifo vya akina mama vitokanavyo na matatizo ya uzazi.

- Kuongezeka kwa asilimia ya kaya zilizojiunga na mfuko wa afya ya jamii (CHF) kufikia 11%.

- Kufungua na kuanza kutoa huduma kwa wananchi zahanati tano (5) katika vijiji vya Mang'hweta, Tubugwe juu, Mseta Bondeni, Chang'ombe na Chamae.

- Kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto chini ya miaka mitano ambapo mpaka sasa watoto **67,850** kati ya **60,918** sawa na **111.4%** wamesha sajiliwa na kupata vyeti.

- Kukamilika kwa majengo matatu ya hospitali ya wilaya (maabara, upasuaji na stoo ya dawa) kwa 100% na kuanza kutoa huduma.

- Kuchimba kisima kirefu cha maji kwa ajili ya matumizi ya kituo cha afya Mbande kwa kushirikiana na wadau.

Halmashauri inatoa shukran za dhati kwa Mkurugenzi wa kampuni ya ***Hydrotech Tanzania Limited*** ndugu ***Wilson Mgombela*** kwa namna alivyojitolea mitambo yake bila gharama kuchimba kisima hicho ambapo Halmashauri imechangia mafuta kwa ajili ya zoezi hilo.



*Zoezi la uchimbaji wa kisima kirefu cha maji katika kituo cha Afya Mbande*

# Halmashauri yavuka malengo ya ukusanyaji wa mapato

Moja ya jukumu kubwa la Halmashauri ni kukusanya mapato.

Katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri ilikisia kukusanya kiasi cha shilingi **809,416,750** , lakini hadi kufikia tarehe 30 Septemba, Halmashauri imekusanya kiasi cha shilingi **833,728,156.89** ambayo ni sawa na asilimia **103** ya Makisio ya robo ya kwanza.

Mapato hayo yamejumuisha Mapato halisi ya Halimashauri na Michango ya Jamii. Mapato halisi ya Halmashauri ni Sh. **773,464,848.46** sawa na asilimia **149.48** ya Makisio ya Sh. **517,427,250.00 .**

Mikakati ya Halmashauri ni kuendelea kuboresha vyanzo vyake vya mapato na kubuni vyanzo vipya. Maeneo ya kimkakati ni pamoja na kuboresha miundombinu na usimamizi katika soko la Kibaigwa pamoja na lile la Mkoka. Kuongeza mashine za kukusanyia mapato (POS) na kuongeza udhibiti katika mfumo mzima wa kukusanyia mapato ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi za mara kwa mara katika mfumo mzima wa mapato.

> ***"Matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika kukusanya mapato ni tiba ya kuziba mianya ya upotevu"***

# Kero za wananchi zapatiwa majawabu Kongwa

Toka kuteuliwa kwake mwezi wa saba mwaka huu, mkuu wa Wilaya ya Kongwa Dkt. Suleiman Serera amekuwa akifanya ziara za kata kwa kata kwa lengo la kujitambulisha na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Katika mikutano yake na wananchi, mkuu wa Wilaya amekuwa akiambatana na wakuu wa Idara na taasisi mbalimbali za serikali kutoa majawabu sahihi kwa wananchi.

Pichani ni mkuu wa Wilaya Dkt Serera



mwenye koti la bluu akipitia nyaraka ziliyowasilishwa kwake na mwananchi akilalamika kudhulumiwa haki yake.

Katika mikutano hiyo, kero zilizopatiwa majawabu ni pamoja na zile zinazohusu migogoro ya ardhi, umeme kutokufika katika baadhi ya maeneo, kutokutumika kwa stendi ya Kibaigwa ambayo kwa sasa inafanya kazi na kero nyingine nyingi ambazo zimeundiwa kamati maalum kwa ajili ya kuandaa taarifa ya kina.

# Wadau waungana kuweka mkazo katika kilimo cha Korosho Kongwa

Uchumi wa Wilaya ya Kongwa kwa kiasi kikubwa unategemea mazao na mifugo. Katika kulitambua hilo, Halmashauri inashirikiana na taasisi mbalimbali katika kubuni mazao mbadala ya kiuchumi ili kukuza uchumi wa wilaya kwa ujumla.

Katika kipindi cha robo ya kwanza Halmashauri imeshiriana na watafiti kutoka Kituo cha Utafiti cha Kilimo cha TARI-Naliendele kufanya mafunzo ya siku mbili kwa Maafisa Ugani na wakulima wa mfano wa zao la korosho.

Lengo la mafunzo haya lilikuwa kuwajengea uwezo Maafisa Ugani na Wakulima ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji wa Korosho.

Katika mafunzo haya washiriki walifundishwa kwa Nadharia na Vitendo ambapo mada muhimu walizofundishwa ni pamoja na:-Uanzishaji wa Mashamba mapya, Utambuzi na Udhibiti wa Wadudu waharibifu na Magonjwa ya Mikorosho, Matumizi sahihi ya Viuatilifu na Ubora wa Korosho.



*Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Dkt. Suleiman Serera akifungua mafunzo ya kilimo bora cha korosho.*

Jumla ya washiriki **50** walipata mafunzo haya kwa ajili ya kuwapatia mbinu bora za kutoa huduma kwa wakulima wa zao la Korosho.



*Washiriki wakiendelea kupata mafunzo kwa vitendo.*

Kazi iliyobaki baada ya mafunzo haya ni kufikisha elimu hiyo kwa wakulima wa zao hilo.

Ni mategemeo ya Halmashauri kuwa elimu hii italeta matokeo chanya, hususan katika kuendeleza zao la Korosho katika wilaya ya Kongwa.

# Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu yaendelea vyema Kongwa

Uchaguzi Mkuu kwa nafasi ya Rais, Wabunge na Madiwani utafanyika nchini kote tarehe **28/10/2020.** Maandalizi ya uchaguzi huo yanaendelea vema katika jimbo la Kongwa.

Jimbo la Kongwa lina jumla ya vituo **511** katika kata zote **22**. Idadi ya wapiga kura ni **188,475.** Maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wasaidizi ngazi ya kata, maandalizi ya vifaa mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi na maelekezo kwa vyama vya siasa.



*AROs Kata wakila kiapo kwa ajili ya kusimamia uchaguzi Mkuu.*



*Msimamizi wa uchaguzi katika picha ya pamoja na viongozi wa vyama vya siasa baada ya kuwapa maelekezo.*

# Serikali yatoa milioni 569,506,000 kwa kaya za TASAF

Katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa imepokea fedha kiasi cha shilingi **569,506,000** kwa ajili ya kulipa walengwa wa Mpango wa kunusuru kaya masikini (TASAF).

Kati ya fedha hizo, shilingi **103,150,000** zimelipwa kwa Wasichana Rika Balehe -AGYW na shilingi **466,356,000** kwa walengwa wengine. Fedha hizi zimekuwa mkombozi kwa walengwa wa kaya hizo kwani baadhi yao wamefanikiwa kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato.

Pichani kushoto ni msichana wa rika balehe ***Bitrisi hardison Chigoji*** aliyeanzisha mradi wa ufugaji wa nguruwe na biashara ya uuzaji wa sabuni.

Mpango wa kunusuru kaya masikini (TASAF) katika Halmashauri ya Kongwa unatoa huduma kwa kaya **7,821** katika vijiji **43.** Jumla ya Wasichana **1,875** wa rika balehe (AGYW) wanafaidika na mpango huu.



# Kongwa yajipanga kuzuia upotevu wa mazao kabla na baada ya kuvunwa

Kwa kiasi kikubwa mazao mengi hupotea mashambani kabla ya kuvunwa na hasa kutokana na uharibifu unaosababishwa na wadudu mbalimbali waharibifu na mengine hupotea kutokana na mbinu zisizo bora katika uvunaji kama vile kuvuna na kutupa ardhini.

Aidha wakati wa kusafirisha pia mazao hupotea njiani na hasa kutokana na kutumia vyombo hafifu vya kusafirishia kama vile kusafirisha mahindi kichele kwenye matrekta.

Katika kukabiliana na hilo, Halmashauri imeanza kutoa elimu ya matumizi ya teknolojia mbalimbali za uhifadhi wa mazao kabla na baada ya kuvunwa.

Katika kuhamasisha elimu ya hifadhi bora wa mazao Halmashauri kupitia maafisa ugani wa ngazi zote imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya teknolojia zilizoboreshwa katika kuhifadhi mazao yao baada ya kuvunwa.

Moja ya teknolojia zilizoboreshwa ni mifuko ya kinga njaa (*PICs bag*) ambapo kwa kipindi cha robo ya kwanza takribani mifuko **2000** imeuzwa kwa wakulima na vikundi kupitia maafisa ugani na wauza pembejeo.



*Matumizi ya teknolojia iliyoboreshwa ya kuhifadhi mazao kwa kutumia mifuko ya PICs.*

Matumizi sahihi ya mifuko hii katika kuhifadhia nafaka yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia upotevu wa nafaka hizo unaotokana na wadudu kwani teknolojia inayotumika katika kutengeneza mifuko hii hairuhusu wadudu kuwa na uhai katika mifuko hiyo, hii inatokana na ukweli kwamba mifuko hiyo haipitishi hewa.

Ili kuongeza upatikanaji wa huduma hii ya mifuko wataalam wamehamasisha - wafanyabiashara wenye maduka kuuza mifuko hii ambapo kwa sasa mifuko hii inapatikana kwenye maduka ya nguo, maduka ya vifaa vya ujenzi nk.

Jambo hili ni mafanikio makubwa kwani inaonesha wakulima wengi wamehamasika katika matumizi ya mifuko hii badala ya kutumia viuatilifu ambavyo vina athari za kiafya.



*Uhifadhi wa njia hii si sahihi kwani hupelekea upotevu mkubwa wa mazao*

Elimu zaidi itaendelea kutolewa na hasa tunapoelekea msimu huu wa kilimo.

# Wananchi waendelea kunufaika na mkopo wa 10%

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa imeendelea kutekeleza takwa la kisheria la utoaji wa mikopo kwa makundi maalum ya wanawake, vijana na walemavu.

Jumla ya mikopo yenye thamani ya shs **34,000,000** imetolewa kwa vikundi **3** vya wanawake yenye thamani ya shs. **14,000,000** na Vikundi **2** vya vijana yenye thamani ya shilingi **20,000,000.**

Vikundi viwili vya vijana vilivyopata mkopo wa pikipiki ni kikundi cha ***Kongo*** kutoka kijiji cha Ibwaga kata ya Ugogoni na kile cha ***Boda boda Benki*** kutoka kata ya Kongwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi pikipiki hizo kwa vijana, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Dkt. Suleiman Serera aliwaasa vijana kuzingatia kanuni za usalama barabarani ili kuepusha ajali zitakazo sababisha upotevu wa maisha na uharaibifu wa mali.

Aidha aliwataka kuwa mabalozi wazuri wa ulinzi na usalama wa Wilaya kwa ujumla. Mkuu wa Wilaya alisema

*"Ninyi madereva wa Boda boda mnalo jukumu kubwa katika kulinda usalama wa wilaya kutokana na kazi yenu mnayoifanya. Ninyi mnabeba abiria wa aina tofauti, wengine ni watu wema na wengine si watu wema. Ukiwa na mashaka na abiria uliyembeba toa taarifa kwa vyombo vya ulinzi ili hatua stahiki zichukuliwe"*




*Mkuu wa Wilaya ya Kongwa Dkt. Suleiman Serera akikabidhi pikipiki kwa vijana ikiwa ni mkopo wa asilimia kumi*

Mkuu wa Wilaya aliwakumbusha wanachama wa vikundi hivyo kurejesha mikopo hiyo kwa wakati ili fedha hizo zitumike kukopesha vikundi vingine.

Aidha akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wanachama wa vikundi hivyo vilivyopata mkopo, ndugu Baraka Kusudya alimshukuru Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyowajali wananchi wake kwa kuwawezesha mikopo isiyokuwa na riba kwani mikopo hiyo itawainua kiuchumi.

Bwana Baraka aliwaasa vijana wenzake kuzitunza na kuzilinda pikipiki hizo kwani kwa upya wake, hata wezi wanazinyemelea.

Aidha katika robo ya kwanza Halmashauri imefuatilia urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa kwa makundi mbalimbali na kiasi cha shilingi **12,267,000** zimerejeshwa.

Fedha hizi zimerejeshwa na Vikundi vya Vijana shilingi **2,862,000** vikundi vya wanawake shilingi **8,405,000** ,na walemavu shilingi **1,000,000.** Wananchi wote waliokopeshwa fedha hizo wanahimizwa kuzirejesha kwa wakati.